**MPC NA.242** **2 Aprili 2026**

## Tamko la Kamati ya Sera ya Fedha

Kamati ya Sera ya Fedha (MPC) ilifanya kikao cha kawaida, jana, tarehe 1 Aprili 2026, kufanya tathmini ya mwenendo wa uchumi na Riba ya Benki Kuu (Central Bank Rate-CBR). Kutokana na tathmini hiyo, Kamati iliamua kiwango cha Riba ya Benki Kuu kubaki asilimia 5.75 kwa robo ya pili ya mwaka 2026. Kiwango hicho kilionekana ni sahihi kwa sasa katika kudhibiti mfumuko wa bei kubakia ndani ya lengo la asilimia 3 hadi 5. Aidha, kiwango hicho kitawezesha kupunguza athari za mgogoro wa kisiasa unaoendelea Mashariki ya Kati kwenye uchumi wa nchi yetu. Mgogoro huo umeathiri biashara, uwekezaji, na ustahimilivu wa uchumi wa dunia.

Aidha, Kamati imeamua kupunguza wigo wa riba ya Benki Kuu kutoka asilimia +/-2 hadi asilimia +/-1.5, kuanzia mwezi Aprili 2026. Lengo la hatua hii ni kuboresha ufanisi wa utekelezaji wa sera ya fedha katika kuhakikisha mfumuko wa bei unabaki ndani ya lengo na kuchochea ukuaji wa uchumi. Kufuatia uamuzi huu, wigo wa riba ya mikopo ya siku 7 baina ya benki utakuwa kati ya asilimia 4.25 hadi asilimia 7.25 kwa robo ya pili ya mwaka 2026. Hivyo, Benki Kuu itatekeleza sera ya fedha kwa lengo la kuhakikisha kuwa riba ya mikopo ya siku 7 baina ya benki inabaki ndani ya wigo huo.

### Tathmini ya hali ya uchumi wa dunia

Katika kutathmini mwenendo wa uchumi wa dunia, Kamati ilibaini kuwa ukuji wa uchumi wa dunia ulitarajiwa kuendelea kuimarika kwa mwaka 2026. Hata hivyo, matarajio ya mwenendo huu wa uchumi yanaweza kuathiriwa na kuongezeka kwa mgogoro wa Mashariki ya Kati hivi karibuni, hali inayovuruga mnyororo wa ugavi na kusababisha ongezeko la bei za bidhaa duniani. Mfumuko wa bei katika nchi nyingi ulikuwa mdogo, hata hivyo, kuna uwezekano wa kuongezeka kutokana na kupanda kwa bei za nishati na ongezeko la gharama za usafirishaji.



16 Barabara ya Jakaya Kikwete, S.L.P. 2303, 40184 Dodoma - Tanzania,

Barua Pepe: info@bot.go.tz, Tovuti: www.bot.go.tz, Simu: +255 22 223 2541/2501

Mathalan, bei ya mafuta ghafi, ambayo ilitarajiwa kubaki katika wastani wa dola za Marekani 60 kwa pipa katika robo ya kwanza ya mwaka 2026, ilipanda na kuvuka dola za Marekani 100 kwa pipa. Katika mazingira haya, benki kuu katika nchi mbalimbali zinaweza kulazimika kubadili mwelekeo wa sera ya fedha ili kudhibiti mfumuko wa bei endapo mgogoro wa Mashariki ya Kati utaendelea kwa muda mrefu.

**Tathmini ya hali ya uchumi wa ndani**

Kamati ilibaini kuwa mgogoro unaoendelea Mashariki ya Kati unaweza kuwa na athari kubwa katika uchumi wa ndani. Hata hivyo, hadi sasa ukuaji wa uchumi umeendelea kuwa thabiti, ambapo katika robo ya kwanza ya mwaka 2026 ukuaji wa uchumi kwa Tanzania Bara unakadiriwa kufikia asilimia 6.2 na asilimia 6.7 kwa Zanzibar. Ukuaji huu umechangiwa zaidi na shughuli za ujenzi, kilimo, huduma za fedha na bima, pamoja na utalii. Aidha, mikopo kwa sekta binafsi imeendelea kukua kwa kasi ya kuridhisha, kufikia wastani wa asilimia 22.8, sambamba na ongezeko la mahitaji ya mikopo kwa wafanyabiashara na watu binafsi. Katika robo ya pili ya mwaka 2026, uchumi wa Tanzania Bara na Zanzibar unatarajiwa kukua kwa asilimia 6.1 na asilimia 6.6, mtawalia. Hata hivyo, kuendelea kwa mgogoro wa Mashariki ya Kati kwa muda mrefu kunaweza kupunguza matarajio ya kasi hii ya ukuaji wa uchumi.

Mfumuko wa bei uliendelea kuwa ndani ya lengo kufikia wastani wa asilimia 3.3 katika robo ya kwanza ya mwaka 2026 kwa Tanzania Bara na asilimia 4.5 kwa Zanzibar, kutokana na utekelezaji thabiti wa sera ya fedha pamoja na utulivu wa bei za chakula na nishati. Hali hii inaashiria kuwa athari za awali (*first-round effects*) za ongezeko la hivi karibuni la bei za nishati na gharama za usafirishaji bado hazijaanza kuonekana kwenye mfumuko wa bei. Aidha, athari za kupanda kwa mfumuko wa bei kutokana na gharama kubwa za nishati na usafirishaji inatarajiwa kupunguzwa na utulivu wa bei za chakula nchini pamoja na uthabiti wa thamani ya shilingi. Hivyo basi, Kamati inatarajia kuwa mfumuko wa bei katika robo ya pili ya mwaka 2026, utaendelea kubaki ndani ya lengo la asilimia 3 hadi 5.

Sekta ya benki iliendelea kuwa thabiti, ikiwa na ukwasi wa kutosha na mtaji inaoweza kuhimili vihatarishi. Ubora wa mikopo uliendelea kuimarika kutokana na mazingira wezeshi ya biashara


16 Barabara ya Jakaya Kikwete, S.L.P. 2303, 40184 Dodoma - Tanzania,
Barua Pepe: info@bot.go.tz, Tovuti: www.bot.go.tz, Simu: +255 22 223 2541/2501

na usimamizi madhubuti wa vihatarishi, ambapo uwiano wa mikopo chechefu uliendelea kupungua hadi kufikia asilimia 2.9, chini ya kiwango cha juu kinachovumilika cha asilimia 5. Mifumo ya malipo pia imeendelea kufanya kazi kwa ufanisi.

Urari wa malipo ya kawaida uliendelea kuimarika, ambapo unakadiriwa kufikia nakisi ya asilimia 2.2 ya Pato la Taifa kwa mwaka unaoishia Machi 2026, kutoka asilimia 2.4 mwaka 2025, licha ya kuongezeka kwa mgogoro wa kisiasa Mashariki ya Kati. Mwenendo huu umetokana na ongezeko la mauzo ya nje ya nchi, hususan dhahabu, utalii na bidhaa za kilimo. Urari wa malipo ya kawaida kwa upande wa Zanzibar uliendelea kuwa na ziada kutokana na ongezeko la mapato ya utalii. Thamani ya shilingi dhidi ya fedha za kigeni iliendelea kuimarika, ikichangiwa na uwepo wa akiba ya kutosha ya fedha za kigeni inayozidi dola za Marekani bilioni 6.2 inayotosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kwa miezi 4.8. Kiwango hiki ni juu ya ukomo wa chini wa kisheria wa kuanzia miezi 4 na kigezo cha mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) cha kuanzia miezi 4.5.

Kamati iliridhishwa na mwenendo wa utekelezaji wa sera ya bajeti, ambapo makusanyo ya kodi yalivuka lengo, yakiakisi ukuaji wa shughuli za kiuchumi, kuendelea kuimarika kwa ufanisi wa usimamizi wa kodi, pamoja na ongezeko la ulipaji kodi kwa hiari. Aidha, matumizi ya Serikali yaliendelea kuwiana na rasilimali zilizopo.

Kamati ilihimiza Benki Kuu kuendelea kufanya tathmini ya kina kuhusu mwenendo wa mgogoro unaoendelea Mashariki ya Kati pamoja na athari zake kwa uchumi wa nchi yetu. Kikao kijacho cha Kamati ya Sera ya Fedha kinatarajiwa kufanyika Julai 2026.

**Emmanuel M. Tutuba**
**GAVANA**



16 Barabara ya Jakaya Kikwete, S.L.P. 2303, 40184 Dodoma - Tanzania,
Barua Pepe: info@bot.go.tz, Tovuti: www.bot.go.tz, Simu: +255 22 223 2541/2501